



Kutayarisha mimea chipukizi



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Watayarishaji:

Nasambu O., Talam P.,
Kidula N. na Mwariri M.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkuu wa Kituo,

KARI-Kisii

SLB 523, Kisii, 40200

Simu: (058) 31800/1/2/3 au 058 31800

Baruapepe: kari-kisii.weternet.co.keu@salpha.co.ke

Kisii-kari@yahoo.com

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 32 /2008

Shilingi 20 za Kenya

**Jinsi za kuzalisha mbegu ya
ndizi kutokana na mimea
iliyoko shambani**



Utangulizi

Ndizi ni mmea muhimu wa chakula nchini Kenya lakini ukuzaji wake umezorota kwa sababu ya hali duni ya mpangilio wa kukuza, magonjwa, wadudu na pia ukosefu wa mimea ya kupandia.

Mimea safi vya kupandia ni nini?

Hii ni mimea isiyo na wadudu wala maradhi.

Kwa nini tutumie mimea safi ya kupandia?

- Ili kupunguza uenezaji wa wadudu na maradhi.
- Ili kupunguza utumizi wa madawa katika kuangamiza maradhi na wadudu.
- Kukuza ndizi kubwa na bora zaidi.
- Kupata bei bora kwenye soko.
- Kuleta faida ya kifedha kutokana na uuzaji wa mbegu.
- Kuimarisha mapato ya kijamii.

Mbegu safi ua mandizi hupatikana wapi

Mashamba ya mimea ya ndizi yenye afya na isiyo na wadudu

Jinsi ya kutayarisha mbegu safi za kupandia

Baada ya kuchagua aina za ndizi zinazohitajika, tayarisha mbegu kama ifuatavyo:

a) Sword sucker (mmea mchanga wenye majani membamba)


Chagua mmea wenye urefu wa futi moja hadi tatu wenye afya na majani membamba.

b) Maiden sucker (mmea wenye majani mapana)

Chagua mmea wa mita moja unusu (futi nne na nusu) kwa aina zile refu na mita moja (futi tatu) kwa aina za wastani.

c) Mbinu ya kutayarisha mbegu

Baada ya kung'oa mmea, toa mizizi yote na sehemu zote zenye ishara ya wadudu au maradhi katika kiini cha mbegu.



Toa mizizi na sehemu zilizoathirika

Kutayarisha mbegu kwa kutumia maji moto

Chemsha maji mpaka yafikie nyuzi 55 na udhihirishe kwa kutumia mshumaa ulioshikiliwa kwa kijiti ambao huyeyuka utiwapo ndani ya maji.




Maji yakichemka



Kupima kwa mshumaa

Toa maji kwenye moto na utumbukize mbegu ndani yake kwa muda wa dakika ishirini.




Kulowesha shina kwenye maji moto

Kupanda mbegu kwenye chombo

- Jaza unga wa mbao (saw dust) kwenye pipa robo au chombo kingine chenye kina kama hicho kisha unyunyizie maji.
- Tia mbegu zilizotumbukizwa kwa maji moto katikati mwa chombo na uhakikishe unga wa mbao umefunika kiini vizuri.




Mmea chipukizi safi



Mmea kwenye Chombo

- Baada ya siku sita angalia kama mimea chipukizi inaota kutoka kwa kiini.



Mimea chipukizi ikiota

- Nyunyizia maji kila siku kwa muda wa wiki mbili au mpaka mimea chipukizi iwe tayari kuhamishiwa shambani.